

**What works best: 2020 update**

**Overview of research into best teaching practices**

**Information for parents and carers of school students**

# Kinachofanya kazi bora: Sasisho la 2020

## Maelezo ya jumla ya utafiti juu ya mazoea bora ya kufundisha

### Habari kwa wazazi na walezi wa wanafunzi wa shule

Shule za serikali za NSW zimejitolea kuhakikisha kuwa jinsi tunavyomfundisha mtoto wako inategemea kile kinachofanya tofauti kubwa kwa kujifunza kwake.

Mnamo 2020 Idara ya Elimu ya NSW ilitoa sasisho la baadhi ya utafiti wa muhimu zaidi kuhusu ufundishaji mzuri. Ripoti hii inaitwa 'Kinachofanya kazi bora: Sasisho la 2020' na inaeleza mazoea nane yanayotegemea ushahidi ambayo waalimu wanaweza kutumia katika masomo yao ili kusaidia wanafunzi kuboresha kujifunza. Kuna uwezekano kwamba kile 'Kinachofanya kazi bora: Sasisho la 2020' kitajulisha ufundishaji na ujifunzaji katika shule ya mtoto wako kwa miaka ijayo.

Chini ni muhtasari wa mazoea nane ya 'Kinachofanya kazi bora' kwa ufundishaji mzuri, pamoja na vidokezo vya mazungumzo kukusaidia kuunga mkono mazoea haya nyumbani. Tunadokeza kwamba utumie seti moja ya maswali kwa wakati mmoja na mtoto wako.

Unaweza kupata chapisho cha 'What works best: 2020 update', pamoja na nyenzo zingine zinazotegemea ushahidi kwa shule, kwa education.nsw.gov.au/about-us/educational-data/what-works-best-2020-update

### 1. Matarajio makubwa

Wanafunzi hujifunza vizuri sana wakati walimu wana matarajio makubwa. Kuwa na matarajio makubwa kuna maana kwamba walimu wanafanya kazi kwa bidhii ili kuvutia maslahi ya wanafunzi, kuwatia moyo kujifunza mambo mapya, kutoa msaada wanaohitaji, ni wazi na waaminifu kuhusu jinsi wanavyotaka wanafunzi kutendea na kujifunza, na wanabadilisha jinsi wanavyofundisha kuridhi mahitaji ya wanafunzi.

**Zungumzia na mtoto wako**

- Kwa wanafunzi wa shule ya msingi: Je, unamwonyeshaje mwalimu wako kile unachojua na kile unachoweza kufanya?
- Kwa wanafunzi wa sekondari: Mwalimu wako anahitaji kufahamu umefikia wapi katika kujifunza kwako, ili wajue cha kufundisha baadaye. Je, unamwonyeshaje mwalimu wako kile unachojua na kile unachoweza kufanya?

### 2. Mafundisho ya wazi

Wanafunzi wanajifunza vizuri zaidi wakati kufundisha ni wazi, hasa wakati wanapojifunza kitu kipya. Mafundisho ya wazi kunahusisha waalimu wakieleza wazi kwa wanafunzi sababu wanajifunza jambo, jinsi linavyounganisha na vingine wamevijifunza tayari, wanavyotarajia wanafunzi kufanya, jinsi wanavyofanya na inavyoonekana wakati wamefanikiwa.

**Zungumzia na mtoto wako**

- Kwa wanafunzi wa shule ya msingi na ya sekondari: Niambie kuhusu kitu ulichojifunza leo. Je, uliona ni rahisi kujifunza, au ulihitaji kuuliza maswali machache? Unawezaje kusema wakati 'umeelewa'?

### 3. Maoni mazuri

Wanafunzi wanajifunza vizuri sana wakati waalimu wanapowapa maoni mazuri. Maoni ambayo ni bora ni ya kujenga, ya kina na maalum. Inazingatia jinsi wanafunzi walivyofanya kazi fulani, na iko wazi juu ya wapi makosa yalifanywa na ni nini kinahitaji kutokea ili kuboresha baadaye.

**Zungumzia na mtoto wako**

- Kwa wanafunzi wa shule ya msingi na ya sekondari: Unapojifunza kitu kipya, unajuaje ikiwa uko kwenye njia sahihi? Unajuaje unachoweza kufanya ili kuboresha wakati ujao?



NSW GOVERNMENT

## 4. Matumizi ya data kufahamisha mazoea

Wanafunzi hujifunza vizuri wakati waalimu wanapotumia data kuthibitisha wanafunzi wako wapi kwenye masomo yao na kupanga nini cha kufundisha baadaye. Data ni aina yoyote ya habari ambayo husaidia waalimu kufanya hivyo. Data zinaweza kutoka kwa anuwai ya maeneo, pamoja na maswali ya darasa, majibu ya wanafunzi kujibu maswali ya mwalimu, sampuli za kazi za wanafunzi na mitihani rasmi.

## 5. Tathmini

Wanafunzi hujifunza vizuri wakati walimu wanapotumia tathmini ya hali ya juu. Tathmini inahusu anuwai ya shughuli ambazo waalimu hutumia kutathmini ni wapi wanafunzi wako katika masomo yao. Inajumuisha shughuli rasmi kama mitihani na tafiti, na pia shughuli zisizo rasmi kama vile kuuliza maswali ya wanafunzi na kutathmini sampuli za kazi zao.

### Zungumzia na mtoto wako

- Kwa wanafunzi wa shule ya msingi: Je, unamwonyeshaje mwalimu wako kile unachojua na kile unachoweza kufanya?
- Kwa wanafunzi wa shule ya sekondari: Mwalimu wako anahitaji kuelewa uko wapi katika ujifunzaji wako, ili aweze kujua nini cha kufundisha baadaye. Je, unamwonyeshaje mwalimu wako kile unachojua na kile unachoweza kufanya?

## 6. Usimamizi wa darasa

Wanafunzi hujifunza vizuri zaidi wakati walimu wanasimamia madarasa yao vizuri. Usimamizi wa darasa ni pamoja na anuwai kubwa ya vitu ambavyo waalimu hufanya kuhamasisha mazingira salama, mazuri na ya kuchochea ya wanafunzi wao.

### Zungumzia na mtoto wako

- Kwa wanafunzi wa shule ya msingi: Je, kuna sheria au matarajio unayohitaji kufuata darasani kwako? Unaweza kuniambia machache? Ni nini hufanyika unapojitahidi kufuata? Ni nini hufanyika ikiwa hautawafuata?
- Kwa wanafunzi wa shule ya sekondari: Je, shule yako ina sheria au matarajio ya shule au ya darasa? Unaweza kutaja chache? Ni nini hufanyika wakati wanafunzi wanayafuata? Ni nini hufanyika ikiwa wanafunzi hawatawafuata?

## 7. Ustawi

Wanafunzi hujifunza vizuri wanapokuwa na kiwango cha juu cha ustawi. Ustawi wa mwanafunzi ni neno pana ambalo linajumuisha afya nzuri ya kiakili, ya kimwili na ya kihemko, kuhisi kuungwa mkono katika kujifunza, kujenga uhusiano mzuri na kuwa na maana na kusudi kwenye nguvu. Walimu wanaweza kusaidia ustawi wa wanafunzi kwa:

- kujenga mazingira salama
- kusaidia wanafunzi kuhisi kuwa wao ni mali
- kuthamini maoni na mitazamo yao
- kuwahimiza wawe na hamu ya kujifunza
- kuwasaidia kusimamia hisia zao
- kuwasaidia kukuza uhusiano mzuri na waalimu na wanafunzi wengine.

### Zungumzia na mtoto wako

- Kwa wanafunzi wa shule ya msingi na ya sekondari: Je, unajisikiaje kuhusu shule kwa sasa? Je, kuna mambo ambayo unaona ni vigumu au changamoto? Je, unajua cha kufanya au ni nani unaweza kuzungumza naye ikiwa una siku mbaya au una shida? Je, kuna mtu anayekujali shuleni?



## 8. Kushirikiana

Wanafunzi hujifunza vizuri wakati walimu wanashirikiana. Ushirikiano unajumuisha walimu kufanya kazi pamoja na walimu wengine na wataalam kutoka nje ya shule ili kuboresha ufundishaji wao. Ushirikiano unaofaa unaweza kujumuisha walimu wanaopanga masomo na mipango ya kufundisha pamoja, kuangaliana masomo yao na kupeana maoni, na kujadili na kufikiria juu ya maswala yanayohusiana na kazi zao.

### Kwa mfano...

#### Matarajia makubwa kwa Aldavilla Public School

Aldavilla Public School inaonesha mafanikio yake mengi katika kuboresha matokeo kwa wanafunzi kuzingatia matarajio makubwa. Wanafunzi wanakumbushwa kila wakati kuwa wanaweza kuwa chochote wanachotaka kuwa. Njia moja ambayo matarajio makubwa yanahimizwa katika Aldavilla Public School ni kupitia kuweka malengo. Wanafunzi wanatarajiwa kufanya kazi kufikia malengo ya kujifunza ambayo yanaweza kutekelezwa, na wafanyakazi wanahimiza kila wakati wanafunzi kujisukuma kufikia lengo lao lifuatalo.

Shule pia inahimiza matarajio makubwa kwa kuchukua njia ya shule nzima. Kwa mfano, kila darasa hufuata mfumo sawa wa usimamizi wa tabia. Uhusiano wa mwanafunzi na mwalimu pia ni kipaumbele. Walimu wote wanajitahidi kuwajua wanafunzi na kuonyesha kuwa wanawajali. Hii inaweza kupatikana kwa kufanya vitu rahisi kama kuuliza kile wanafunzi walifanya mwishoni mwa wiki, au kujua ndugu na dada wa mwanafunzi ni akina nani.

### Kwa mfano...

#### Matumizi ya data kufahamisha mazoea katika Concord High School

Kitivo cha hisabati katika Concord High School huangalia data zao za HSC kila mwaka na hutumia matokeo kupanga mipango yao ya kufundisha katika Years 7-11. Mwalimu mkuu wa hisabati anaelezea: "Tuna mtazamo mzuri wa maswali ambayo wanafunzi walikosea na tunajaribu kupanga upya kulingana na mambo ambayo watoto wamekosea. Kwa mfano, wanafunzi wetu walikuwa wakipambana na 'significant figures' ('takwimu muhimu') katika HSC kwa hiyo sasa tumeingiza 'takwimu muhimu' katika Year 7. Hiyo inamaanisha wana miaka sita ya kujifunza jinsi ya kukadiria kutumia 'significant figures.' Sasa 'significant figures' sio suala."

Wakati mwingine programu mpya inajumuisha kubadilisha mpangilio wa mada wakati wa mwaka ili wanafunzi wawe na fursa zaidi ya kutumia maarifa na ufahamu wao wa dhana hizi kwa mwaka mzima. Mwalimu mkuu wa hisabati anaendelea: "Wanafunzi wetu walikuwa wakifanya vibaya sana na 'probability' (uwezekano). Tulitazama mipango yetu na 'probability' ilikuwa kitu ambacho tulikuwa tukifanya kila mwisho wa mwaka, kwa hivyo tumeihamisha kidogo kwa hivo wanaiona mapema katika miaka kadhaa."

### Huduma ya Mkalimani wa Simu

Ikiwa unataka maelezo zaidi tafadhali upigie simu mwalimu mkuu wa shule yako. Ikiwa unahitaji mkalimani kukusaidia na swali lako, tafadhali upige simu Huduma ya Mkalimani wa Simu kwenye 131 450 na uombe kwa mkalimani katika lugha yako. Mwambie mpokeaji simu nambari ya simu unayotaka kupiga simu na mpokeaji simu atapata mkalimani kwenye simu ili kukusaidia na mazungumzo. Hutalipa kwa huduma hii.